



LOWELL PUBLIC SCHOOLS
Henry J. Mroz Central Administration Offices
(Ofisi za Usimamizi wa Kati)
155 Merrimack Street
Lowell, MA 01852

Aprili 17, 2020

Wapenzi familia wa Shule za Lowell Public Schools,

Tunatarajia ya kwamba nyinyi na wapendwa wenu mko salama na wenyе afya katika wakati huu mgumu. Tuko karibu kuingia wiki yetu ya 6 tangu tufunge shule kwa sababu ya janga la COVID-19. Katika hali ya kawaida tungekuwa tunajitayarisha kwa likizo ya Aprili – safari ya familia, kutazama Riadha ya Boston, au kufurahia kupumzika tu. Kwa bahati mbaya, matokeo ya sasa ni mbali sana kuliko kawaida. Kwa kuzingatia usumbu wengi katika masomo ambazo familia zetu wamekabili katika hali hii, tumechukua uamuzi kuendelea na mafunzo ya mbali wiki ijayo ili kulinda taratibu na mifumo mlizoanzilisha ili kutegemeza mafunzo kutoka nyumbani. Pendekazo la kuendeleza mafunzo ya mbali ndani ya likizo ya Aprili ilifanyika baada ya ushauri na washikadau wengi, na uamuzi ulikubaliwa katika mkutano wa Kamati ya Shule uliyofanyika Aprili tarehe 15.

Jumatatu, Aprili 20 ni likizo la Patriots' Day, ambalo ni likizo la serikali, na itazingatiwa kama "siku ya pumziko" kutoka shule. Kwa hivyo shule zote na ofisi zote za wilaya zitafungwa siku ya Jumatatu, halafu mafunzo ya mbali yataanza kutoka siku zitakazofuata wiki ijayo, Jumanne hadi Ijumaa (Aprili 21-24). Tafadhali kumbuka ya kwamba huduma ya chakula itaendelea katika nyakati na maeneo zao za kawaida wiki ijayo, hata siku ya Jumatatu. Orodha kamili ya maeneo na nyakati ya huduma yetu ya chakula inaweza kupatikana katika tovuti ya wilaya.

Mnamo Jumatatu, Aprili tarehe 6, tumebadilisha programu yetu ya elimu kutoka shughuli za kujifunza nyumbani **ya hiari** na kuibadilisha kwa kazi za nyumbani **zinazohitajika** na zitawekwa alama na kurekodiwa katika kadi ya ripoti. Mfumo wetu wa alama utafuata pendekazo la Idara ya Elimu ya Msingi na Elimu ya Upili ya Massachusetts au Massachusetts Department of Elementary and Secondary Education (DESE) ili kubadilisha mfumo kwa "kufaulu/kutofaulu" kutoka mfumo wa 0-100. Tunatambua, haswa katika kiwango cha shule ya upili, kwamba kuhama kwa mfumo kufaulu/kutofaulu, unafaa tushughulikie masuala ya kuhesabu matokeo ya wastani wa kiwango cha daraja (GPA), ambalo huamua tuzo la heshima, ustahiki katika programu za heshima na ufadhilli wa masomo fulani, na ustahiki katika kushiriki katika shughuli fulani za wanafunzi kama riadha, Pamoja na programu zingine za shule. Tutaendelea kukuarifu fursa zinapotengenezwa kukabili masuala haya yanayohusika na GPA.

Katika muda huu wa mafunzo ya mbali, tunawashauri wanafunzi kujishughulisha katika mafunzo yenye malengo na yenye mafanikio kwa takriban nusu ya wakati wa siku ya shule ya kawaida (masaa 3 hadi 3.5). Hili litawezekana kuititia muungano wa shughuli zinazoelekezwa na mwalimu pamoja na shughuli zinazofanyika na mwanafunzi peke yake. Mipango ya mafunzo ya kiwango cha darasa na mapendekazo huchapishwa kwa tovuti la wilaya. Shule zetu zimewasiliana na familia katika kutekeleza wa mafunzo ya mbali. Iwapo hujawasiliana na shule yako, tafadhali pigia shule yako moja kwa moja na hakikisha kwamba taarifa yako ya mawasiliano ni ya sasa.

Tunatambua kwamba mafunzo ya mbali hayawezi kubadilisha masomo ya siku ya shule ya kawaida, lakini tunaendelea na nia ya kutoa mazoeufu ya masomo yenye maana kwa wanafunzi wote wa LPS katika mbinu zinazofaa kuwatia fahari nyingi jamii ya Lowell. Walimu, viongozi wa shule na wafanyakazi

katika kila shule yetu wana shukrani yangu ya dhati, pamoja na wazazi na familia wanaosaidia wanafunzi wetu katika hali hizi ngumu.

Wafanyakazi wa shule yetu wanaendelea kuwasiliana na familia ili kuhakikisha upatikanaji wa mtandao na vifaa nya kiteknolojia kwa kila mtoto yanayohitajika ili kushiriki katika programu ya mafunzo ya mbali. Tafadhalii wasiliana na shule yako iwapo una maswali yanayohusiana na mahitaji yako ya mafunzo ya mbali kama uwezo wa kupata kifaa au mtandao.

Vipengele kadhaa muhimu zimeorodheshwa hapa chini, na tutaendelea kukuarifu pindi habari mpya inapopatikana:

- DESE imetangaza kwamba sharti la kufanya mtihani wa Mfumo wa Tathmini wa Kikamilifu wa Massachusetts au Massachusetts Comprehensive Assessment System (MCAS) limeondolewa kwa mwaka wa shule wa 2019-2020. Hili linamaanisha kwamba wanafunzi wetu katika darasa za 3-10 hawatafanya mtihani iliyopangwa na serikali ambayo ilipangwa kufanyika katika majira haya ya spring. Pamoja na hayo, sharti ya uwezo kwa shule za upili iliyo na msingi na matokeo ya MCAS inaweza kubadilishwa au kuondolewa mwaka huu.
- Kuhitimu shule ya upili kwa sasa imepangiwa kwa kalenda ya mwaka wa shule wa 2019-2020 kutendeka Juni tarehe 3. Kwa sababu ya hali inayoendelea sasa, Juni tarehe 24 imetambuliwa kama tarehe ya dharura inayowezekana. Uongozi wa Lowell High School pia inakutana na afisa wa madarasa ili kuamua tarehe za dharura na mipango za densi ya kuhitimu shule.
- Wakati wa kujisajili wa shule za chekechea zimehairishwa na Ofisi ya Rasilimali ya Familia sasa inachunguza mbinu za kuanzisha upya usajili katika namna salama na iliyofaa. Tutakupatia maelezo zaidi pindi tarehe mpya za usajili zikiamuliwa.

Tutaendelea kuwa nawe na kukusaidia katika muda huu mgumu na tutaendelea kukujulisha katika hali hii. Wakati huohuo, iwapo unahitaji usaidizi zaidi, unaweza kupiga nambari kuu ya shule yako au Kituo cha Rasilimali ya Familia ukipitia nambari hii 978-674-4321. Unaweza pia kuwasilisha swali lako au ombi lako ukipitia fomu hili la mtandao:

<https://docs.google.com/forms/d/e/1FAIpQLSe3Md1leOCZiQ2bi2enmSvUXvROSnPVDPTIs9nmIdFPq3wl5Q/viewform>

Kaa kwa afya na usalama.

Wako,



Dr. Joel D. Boyd
Msimamizi wa Mashule